# pspTB na matukio

Dodoma - Tanzania

Toleo Na 01- Desemba 2024





## PSPTB yaendelea kuhamasisha wanafunzi kujisajili ili kuongeza idadi ya wataalam wa ununuzi na ugavi

## Karibu katika Toleo la Kwanza la Jarida la PSPTB

# Kongamano la 14 la wataalam wa ununuzi lachochea matumizi ya dijitali

# Karibu katika toleo la kwanza la jarida la PSPTB

**Ndugu Msomaji,**

Napenda kutambulisha jukwaa jipya kabisa la habari na kukukaribisha katika toleo jipya la Jarida la PSPTB.

PSPTB inayo furaha kukuletea chapisho ambalo lina lengo la kuhabarisha, kuhamasisha na kushirikisha umma katika kutekeleza majukumu yake katika kusimamia ununuzi na ugavi nchini.

Ni wajibu wetu kuufahamisha umma juu ya mipango yetu, mikakati yetu na maendeleo ya utekelezaji wa kazi zetu katika kufikia malengo tuliyojiwekea kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi.

Katika kufikia malengo yetu, tutahakikisha tunaujulisha umma pamoja na wadau kwa ujumla juu ya changamoto zinazoweza kijitokeza katika utekelezaji wa majukumu yetu ili kujenga uelewa wa pamoja na hivyo kurahisisha utatuzi wa changamoto hizo.

Jarida hili ni kwa ajili ya umma wa Watanzania na wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi kijifunza na kutambua uwepo wa PSPTB kama chombo kinachoweza kuangazia fursa zilizopo na au zinazojitokeza kwa ajili ya maendeleo ya kibiashara, changamoto za ununuzi na ugavi kukiwa na lengo la pamoja la kujenga uchumi imara wa nchi yetu.

Kupitia jarida hili, tutaunganisha sauti za wadau wa sekta ya ununzi na ugavi, watunga sera na watoa maamuzi pamoja na walaji wa mwisho – ambao ndio wanatoa mchango mkubwa katika ununuzi na ugavi hivyo kukuza uchumi wetu.

Jarida hili linalotarajiwa kuchapishwa mara mbili kwa mwaka litatumika kama kipaza sauti au jukwaa la usambazaji wa taarifa zinazohusu ununuzi na ugavi katika kupanua wigo wa uelewa kwa wadau na umma kwa ujumla.

Jarida hili pia linatarajiwa kuongeza thamani kwa shughuli za PSPTB kwa kujenga mawasiliano ya karibu na wadau waliopo na kuwavuta wapya kwenye mnyororo wa sekta ya ununuzi na ugavi ndani na nje ya nchi.

Malengo mengine ya jarida hili yatakuwa kuzijulisha sekta zingine za uchumi kuhusu shughuli za PSPTB, kuwa jukwaa la kubadilishana mawazo kwa ajili ya kukuza sekta ya ununuzi na ugavi pamoja na kutoa habari sahihi kuhusu nafasi ya PSPTB katika kuikuza sekta hii muhimu.

Tunatarajia kwamba wadau wa sekta ya ununuzi na ugavi pamoja na wasomaji wote watakaofikiwa watatupa mrejesho utakaosaidia kuboresha jarida hili kwa manufaa ya maendeleo ya taifa katika kulinda maslahi ya nchi pamoja na kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

Karibu katika safari yetu mpya ya mawasiliano!



**Gedfred Mbanyi**
**Mkurugenzi Mtendaji**




**Picha ya Mbele: Mwigulu Nchemba**
Waziri wa Fedha

## Bodi ya Uhariri

**Bi Shamim A. Mdee**
Mwenyekiti

**Beatrice Sanga**
Katibu

**Dickson Mollel**
Mjumbe



*Washiriki wa Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi wakimpokea Mgeni Rasmi wa ufunguzi wa kongamano hilo, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (MB), Waziri wa Fedha wakati akiwasili ukumbi wa Simba kwa ajili ya ufunguzi.*

# Kongamano la 14 la wataalam wa ununuzi lachochea matumizi ya dijitali



*Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (MB) Waziri wa Fedha akisoma maelezo yaliyoandikwa kwenye Tuzo ya Shukrani aliyokabidhi na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB Ndg. Jacob Jail Kibona kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi wakati wa Ufunguzi wa Kongamano la 14 la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lililofanyika katika Ukumbi wa AICC jijini Arusha.*

**Tarehe 12 hadi 14 December 2023, wataalamu wa Ununuzi na Ugavi kupitia bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPTB), walikutana katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kwenye Kongamano la 14 huku malengo yakiwa kujadili msitakabali wa tasnia hiyo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa.**

Kongamano hilo lilizinduliwa na Waziri wa Fedha Dr. Mwigulu Nchemba ambaye pamoja na mambo mengine aliwasitiza Bodi hiyo kuhakikisha usajili wa wataalam wa tasnia hiyo unafanyika kwa njia ya mtandao ili kuongeza tija na kupunguza milolongo.

"Hatua hii itasaidia kwenye udhibiti wa weledi wa wataalam kuhakikisha wataalam wanaotumia mfumo huu ni wenye sifa za kitaaluma na waliosajiliwa na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi"

Dr. Mwigulu aliwataka PSPTB kuhakikisha wanaendana na dira ya serikali ya kuhakikisha ununuzi unafanyika kwa njia ya mtandao kwa kuzingatia bei halisi ya soko ili kupunguza gharama katika ununuzi wa umma na kuleta tija kwa Taifa katika utekelezaji wa mnyororo wa ununuzi na ugavi nchini.

Kongamano hilo pia lilijadili fursa mbalimbali kwenye tasnia ya ununuzi na ugavi, kubadilisha ujuzi na uzoefu na liliweka malengo na mipango ya namna ya kuwezesha sekta hiyo kufanya kazi kwa ufanisi na tija.

Kongamano hilo la mwaka 2023 lililokuwa na kauli mbiu, 'Mabadiliko ya kidijitali kwa ajili ya kuboresha usimamizi na ugavi kuelekea maendeleo endelevu.' lilihudhuriwa na wataalam mbalimbali kutoka serikalini na sekta binafsi.

Aidha, kongamano hilo lilirekodi ongezeko la washiriki zaidi ya 300 ikilinganishwa na kongamamano la mwaka 2022 ambapo walihudhuria watu 1,517.

# PSPTB yaendelea kuhamasisha wanafunzi kujisajili ili kuongeza idadi ya wataalam wa ununuzi na ugavi

Ikiwa ni sehemu ya Utekelezaji wa mpango mkakati kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) nchini iliandaa ziara ya semina ya uhamasishaji juu ya mambo mbalimbali kwa vyuo vinavyotoa kozi za Ununuzi na Ugavi nchini.

Ziara hiyo iliyoanza shughuli hiyo kati ya mwezi April na May 2024, ilikuwa na malengo ya kuongeza idadi ya watalaam wa sekta ya Ununuzi na Ugavi waliosajiliwa, kuhimiza wanafunzi wanaohitimu masomo hayo kujisajili kwaajili ya mitihani ya kitaaluma pamoja na uanachama.

Viongozi wa PSPTB walifika katika Mikoa minne ambayo vyuo vyake hutoa kozi ya Ununuzi na ugavi ikiwa ni pamoja na Mbeya, Dodoma, Dar es Salaam na Kilimanjaro.

Akiwa ni miongoni mwa viongozi walioshiriki katika ziara hiyo, iliyoandaliwa na Idara ya Masoko na Uhusiano kwa umma kutoka bodi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Bwana Godfred Mbanyi alisema kuwa dunia inabadilika hivyo haina budi wahitimu wa sekta ya Ununuzi na Ugavi kuendana na mabadiliko hayo hususani kwenye suala la uadilifu.

"Ni lazima muwe wazalendo, kwa taifa na taaluma zenu, kuanzia ngazi ya chuo, chuo kikuu, kwenye familia na sehemu ya kazi kwa kauli mbiu moja tu ya Tanzania ni moja na itajengwa na watanzania wenyewe." alisema Bwana Mbanyi.

Ziara hiyo iliyolenga pia kuimarisha uhusiano kati ya PSPTB na vyuo vilivyopo chini yake, ilifanikiwa kufika katika Chuo kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU), Chuo cha Utawala wa Biashara (CBE- Mbeya), Chuo Kikuu cha Science na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo kikuu cha Kikatoliki cha Mbeya (CUoM) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA- Mbeya).

Vyuo vingine vilivyofikiwa na Bodi hiyo kwa kipindi hicho ni kutoka mkoa wa Dar es Salaam, ambavyo ni Dar es salaam Maritime Institute (DMI), Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) na Kilimanjaro Institute of Technology and Management (KITM).

Kwa upande wa Mkoa wa Dodoma ni Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Taasisi ya mafunzo kwa Serikali za Mitaa (LGTI-HOMBOLO) ilihali kwa upande wa Kilimanjaro, chuo kikuu cha Ushirika Moshi (MocU) mafunzo yalichukua nafasi.

Mbali na mafunzo hayo ya uhamasishaji kufanyika katika vyuo hivyo, zaidi ya wanafunzi, 900 wanaosoma masomo ya ununuzi na ugavi kwa ngazi ya Astashahada, Stashada na Shahada na waliosajiliwa kutoka mkoa wa Mbeya walipatiwa mafunzo hayo.

Kwa upande wa Dar es Salaam zaidi ya wanafunzi 899 walipata mafunzo hayo, halikadhalika kwa Mkoa wa Kilimanjaro, zaidi ya wanafunzi 160 walifikiwa huku mkoa wa Dodoma, zaidi ya wanafunzi 500 walipata mafunzo hayo.



*Mwanafunzi wa fani ya Ununuzi na na Ugavi kutoka chuo cha Mwalimu Nyerere Memorial Academy (MNMA) akiuliza swali kwa wataalam kutoka PSPTB mara walipotembelea chuo hicho kwaajili ya kufanya uhamasishaji wa shughuli mbalimbali zinazotolewa na bodi hiyo*

> "Ni lazima muwe wazalendo kwa taifa na taaluma zenu kuanzia ngazi ya chuo, chuo kikuu, kwenye familia na sehemu ya kazi kwa kauli mbiu moja tu ya Tanzania ni moja na itajengwa na Watanzania wenyewe.




*Mgeni Rasmi katika mahafali ya 13 ya mitihani ya kitaaluma ya PSPTB Mhe. Hamad H Chande akizungumza na wahitimu pamoja na wageni mbalimbali waliohudhuria mahafali hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam.*

# Chande aonya wanaofanya Ununuzi, Ugavi bila usajili

> "Tunafahamu kuna baadhi ya Sekta za Umma na Binafsi wana watu wa aina hiyo, wanafanya kazi za kitaaluma za ununuzi bila kutambulika na Bodi yetu hivyo hatutawafumbia macho...

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande amesema serikali itawachukulia hatua watu wanaofanya kazi za kitaaluma za Ununuzi na Ugavi bila ya kusajiliwa na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi nchini (PSPTB)

Kauli hiyo aliitoa aliposhiriki mahafali ya 13 ya Wahitimu wa Mitihani ya Kitaaluma ya Ununuzi na Ugavi yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, Dar es salaam

Alisema serikali haitamvumilia mtu yoyote anayefanya kazi za Kitaaluma pasipo kusajiliwa na bodi na wakibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa

"Tunafahamu kuna baadhi ya Sekta za Umma na Binafsi wana watu wa aina hiyo, wanafanya kazi za kitaaluma za ununuzi bila kutambulika na Bodi yetu hivyo hatutawafumbia macho, tutawashughulikia" Alisema Chande

Chande alitumia nafasi hiyo kuwataka waajiri kutoka Sekta za Umma na Binafsi kuthamini taaluma hiyo kama nyingine na kuwapa kipaumbele katika masuala mbalimbali ya kikaguzi yanayofanyika.

"kumekuwepo na baadhi ya waajiri kufumbia macho mchango wa fani hii, kuruhusu watu wengine wafanye kazi za ununuzi na ugavi bila kutimiza vigezo vya kitaaluma ikiwa ni pamoja na kusajiliwa na Bodi, jambo ambalo sio sawa na halikubaliki "Alisema Chande

Kutokana na hali hiyo chande aliwaagiza wakaguzi kutoka PSPTB kufanya ukaguzi kwa Sekta za Umma na Binafsi ili kuwabaini watu wanaofanya kazi kinyume na utaratibu na sheria zilizowekwa pamoja na kuhakikisha inafanya hamasa vyuoni kuwapata wataalam wengi na wakutosha.

Naye Kamishna wa Ununuzi na Ugavi Nchini Dk Frederick Mwakibinga, aliwataka wahitimu hao kuwa waadilifu na waaminifu katika kazi watakazopata ili kuipa heshima taaluma ya ununuzi ndani na nje ya nchi.

"jiepusheni na tamaa na mridhike na mtakachokipata huko uraiani na pia mtunze heshima ya bodi ikiwa na pamoja na kuitangaza vizuri Bodi yenu" Amesema wakibinga



Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (MB) Waziri wa Fedha akiifurahia Tuzo ya Shukrani aliyokabidhiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PSPTB Ndg. Jacob Jail Kibona kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi wa Ufunguzi wa Kongamano la 14 la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi lilifanyika katika Ukumbi wa AICC jijini Arusha.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano kwa Umma - PSPTB Bi. Shamim Mdee akimshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG Charles Kichere baada ya kutembelea banda la PSPTB wakati wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya ya Dar es Salaam (DITF) (Sabasaba)



Muonekano wa Ukumbi wa Simba AICC-Arusha wakati wa Ufunguzi wa Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi tarehe 12 Disemba. 2023.




Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Bima Zanzibar (ZIC) Ndg. Arafat Haji akipokea Tuzo ya mdhamini mkuu wa kongamano la 14 la Mwaka la wataalam wa Ununuzi na Ugavi kutoka kwa Mgeni Rasmi Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha wakati wa ufunguzi wa kongamano hilo AICC-Arusha.

# Wahitimu wa PSPTB watakiwa kujiendeleza kitaaluma, kuzingatia maadili ya kazi

Wahitimu wa mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Tanzania (PSPTB) wametakiwa kujiendeleza kitaaluma katika nyanja mbalimbali pamoja na kuzingatia maadili ya utendaji kazi, jambo ambalo litaongeza ufanisi kwa maslahi ya taifa.

Akizungumza katika Mahafali ya 13 ya wahitimu wa mitihani ya kitaaluma ya PSPTB, yaliyofanyika Oktoba 19, 2024, katika Ukumbi wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Chande, alisema ni muhimu kwa wahitimu kuendelea kujifunza ili kuimarisha uwezo wao wa kitaaluma na kuboresha utendaji kazi.

Mhe. Chande alisisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili katika taaluma, akiwataka wahitimu kuepuka tabia za wivu, choyo, na husuda ambazo zinaharibu utendaji wa kazi. Pia aliwahimiza kuishi vizuri na watu katika mazingira ya kazi, kuendeleza ushirikiano na kuimarisha uhusiano wa kitaaluma na nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

> "Wahitimu hao ni rasilimali muhimu katika kusimamia na kukagua ununuzi na ugavi kwa kushirikiana na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha, Ofisi za Ukaguzi wa Ndani, mamlaka za umma, na wadau wa sekta binafsi

Mwenyekiti wa Bodi ya PSPTB, Bw. Jacob Kibona, alisema kuwa wahitimu hao ni rasilimali muhimu katika kusimamia na kukagua ununuzi na ugavi kwa kushirikiana na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha, Ofisi za Ukaguzi wa Ndani, mamlaka za umma, na wadau wa sekta binafsi.

Bw. Kibona aliwapongeza wahitimu waliotunukiwa vyeti katika ngazi tatu za taaluma, akisisitiza umuhimu wa kutekeleza kazi kwa kuzingatia maadili ili kulinda heshima ya taaluma na kuleta ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za umma kwa manufaa ya taifa



*Baadhi ya wahitimu wakifuatilia ratiba katika mahafali ya 13 ya wahitimu wa Mitihani ya Kitaaluma ya PSPTB yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, Dar es salaam.*



*Maafisa kutoka Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), wakitoa elimu kwa wataalam walipotembelea banda la Bodi hiyo wakati wa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika tarehe 9-12 Septemba, 2024 katika viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)*



*Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB Bw. Godfred Mbanyi akifafanua jambo kwa Mgeni Rasmi, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dotto Biteko alipotembelea banda la PSPTB wakati wa Ufunguzi wa Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika tarehe 9-12 Septemba, 2024 katika viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC).*



*Baadhi ya maafisa Ununuzi na Ugavi wa Halmashari za Mkoa wa Arusha wakisikiliza kwa makini mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya sheria Mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na Kanuni zake za Mwaka 2024 kutoka kwa wawezeshaji wa PSPTB (hawapo pichani).*




*Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bw. Mcha Hassan akifungua mafunzo ya siku 5 kuhusu Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na Kanuni zake za Mwaka 2024 yaliyoandaliwa na PSPTB kwa watumishi wa TRA.*



*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa PSPTB kwenye picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa kikao cha baraza hilo kilichofanyika mkoani Morogoro.*

# Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wapongeza utendaji kazi wa PSPTB

Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) imefanya kikao cha Baraza la Wafanyakazi mwaka huu ili kujadili mafanikio, changamoto na njia za kuweza kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa bajeti ya mwaka uliopita ya 2023/2024.

Akizungumza kwenye kikao hicho Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalamu Ununuzi na Ugavi Godfred Mbanyi amesema baraza ni chombo kinachoundwa na sheria ya Mahusiano kazini kwa ajili na kuweka mazingira mazuri mahali pakazi ambapo chombo hiki kinawiwa kwa mkataba baina na Menejimenti pamoja na chama cha wafanyakazi sehemu ya kazi.

> "Mabaraza ya kazi kwanza yanaleta ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu ya kazi hivyo wafanyakazi wanakuwa ni sehemu ya maamuzi katika taasisi...

Pia amasema baraza la leo limefanyika ili kutathmini utendaji kazi wa bajeti ya mwaka uliopita ya 2023/2024, kisheria na kiutaratibu bajeti yoyote kabla haijahidhinishwa lazima ipitishwe na Baraza la Wafanyakazi sehemu ya kazi.

Mbanyi amesema Bajeti ya mwaka 2023/2024 ilikamilika toka Juni 30 hivyo ni wajibu wa menejimenti kuja kueleza baraza nini mafanikio, changamoto na njia za kuweza kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa bajeti iliyokamilika muda wake.

"Umuhimu wa Mabaraza ya kazi kwanza yanaleta ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu ya kazi hivyo wafanyakazi wanakuwa ni sehemu ya maamuzi katika taasisi, kwaiyo taasisi sio kwamba inakuwa inaongozwa na Menejimenti lakini inakuwa na chombo ambacho kinawakilisha wafanyakazi wote katika taasisi mbalimbali." Alisema Mbanyi




*Mgeni Rasmi katika mahafali ya 13 ya mitihani ya kitaaluma ya PSPTB Mhe. Hamad H Chande akiwaapisha wahitimu katika mahafali hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam.*



*Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa mafunzo ya ukaguzi wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Bw. Godfred Mbanyi (aliyeketi katikati) pamoja na washiriki na wakufunzi wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa Olasiti Jijini Arusha.*



*Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Missile Musa (Kulia) akipata ufafanuzi wa Jambo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Wa PSPTB Godfred Mbanyi wakati Wa ufunguzi wa mafunzo ya siku mbili ya kuwajengea uwezo maafisa Ununuzi na Ugavi wa halmashari zote za jiji la Arusha ikiwa ni moja ya kurudisha kwa jamii ( CSR) iliyofanyika ukumbi wa Ngorongoro mikoani Arusha tarehe 19 na 20 Novemba, 2024.*



*Wahitimu wa Mitihani ya Kitaaluma ya PSPTB wakiapa mbele ya mgeni rasmi katika mahafali ya 13 ya mitihani hiyo yaliyofanyika katika ukumbi wa JNICC, Dar es Salaam.*

# Zaidi ya watahiniwa 1000 wa ununuzi na ugavi wafanya mtihani



*Watahiniwa wa mitihani ya 29 ya PSPTB wakiwa kwenye chumba cha mtihani. Mitihani hiyo ilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Mwanza na Zanzibar kuanzia tarehe 11 hadi 15 Novemba, 2024.*



Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) imeendesha mitihani yake ya 29 kwa jumla ya watahiniwa 1,223 katika ngazi za Professonal Diploma, Graduate Professional na CPSP.

Mitihani hiyo imefanyika katika mikoa Dar es Salaam, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Mwanza na Zanzibar kuanzia terehe 11 hadi 15 Novemba, 2024.

Akizungumza wakati wa mitihani hiyo ikiendelea, Mkurugenzi wa Mafunzo kutoka Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) Bw. Amani Ngonyani amesema ni muhimu sana kwa wahitimu kutoka vyuo mbalimbali waliosoma masomo ya Ununuzi na Ugavi na wale wanaofanya kazi za Ununuzi serikalini na sekta binafsi ila hawana sifa za kitaaluma kuja kufanya mitihani ya Bodi hiyo ili waweze kupata sifa za kitaalam za kufanya kazi za Ununuzi na Ugavi kwa ubobezi na ufanisi zaidi hili linachagizwa na uwepo wa Mtaala mpya unaowajengea watahiniwa wa PSPTB weledi na umahiri zaidi katika taaluma hiyo.

Bw. Ngonyani amesistiza zaidi kwamba waajiri wasiajiri watumishi katika eneo la ununuzi na ugavi wasiokuwa na sifa stahiki na hususani wale ambao hawajafanya mitihani ya kitaaluma na kuwa na ujuzi na maarifa stahiki.

"Bodi hii iko macho na hatua stahiki za kisheria na kimaadili zitaendelea kuchukuliwa kwa wale wanaokiuka sheria, kanuni na matakwa ya maadili ya Utendaji kazi iwe ni kwa wataalam wa fani ya Ununuzi na Ugavi au wengine wote wanafanya kazi za ununuzi na ugavi pasipo kuwa sifa kwa kuwa kujisajili na kufanya mitihani hii kumerahishwa sana," amesema Ngonyani na ameendekea pia kusema

Haihitaji tena mtu kuja PSPTB ila kwa kutumia simu janja yake au kompyuta yake anaweza kujisajili na kufanya mitihani hii. Aidha tayari kuna baadhi ya vituo vimeanza kutoa mafunzo ya kuwawezesha watahiniwa wa pembezoni au mbali na vituo vya kujifunzia kupata nafasi na fursa ya kusoma hivyo nahimiza wadau wote tushirikiane wakiwemo waandishi wa habari kuhakikisha kazi za Ununuzi na Ugavi zinafanywa na watu wenye sifa za kitaalam na kielimu."

Pia amewasisitiza waajiri wenye watumishi wanaopaswa kufanya mitihani ya kitaaluma ili kuwa sifa zinazohitajika kuwapa ruhusa watumishi hao ili waweze kujiendeleza na pia wawalipie ada za mafunzo na za mitihani ili kuwawezesha watumishi hao kufanya mitihani hii muhimu kwa mustakabali wa utendaji wenye tija katika Taasisi zao.

# WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA PSPTB



Bw. Jacob J. Kibona
(Mwenyekiti)



Wakili. Oscar E. Mangula
(Mjumbe)



Dkt. Alban D. Mchopa
(Mjumbe)



Prof. Michael O. Ndanshau (Mjumbe)



CPA Benezeth K. Ruta
(Makamu Mwenyekiti)



Bi. Esther J. Manyesha
(Mjumbe)



CPA Evaristo O. Mwalongo
(Mjumbe)



Bw. Charles G. Mnyeti
(Mjumbe)

**Jarida hili hutolewa na:**
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB)
Ghorofa ya 7, Mkandarasi Place
S.L.P. 2663, Postcode 41108, Dodoma
Simu: +255 628 903 820

**Nyerere Road, GPSA Premises**
S.L.P. 5993, Dar es Salaam
Simu: +255 22 286 5860
info@psptb.go.tz / barua@psptb.go.tz
www.psptb.go.tz

psptbofficial Bodi Ununuzi PSPTB TV